UTUME WA WASALVATORIANI JUU YA ALAMA ZA NYAKATI

Sr. Dinusha Fernando, SDS

Juni, 2015

Utangulizi

Ulimwengu unabadilika kwa haraka sana. Kila mmoja yupo katika mbio za kufikia malengo yake. Mbio hizo zinakuwa za haraka sana ambapo zinazuia hata muda wa mapumziko na kuona sura za wengine. Kutokana na hili ulimwengu umekuwa ni ardhi iliyochoka na kame. Sheria zote na maadili mema yamepotea. Ulimwengu una kasi kubwa ya kuwa ardhi iliyokavu bila ya maji. Kwa sababu hiyo watu wanamkwepa Mungu. Imani yao imeanguka. Sisi kama Wasalvatoriani tupo hapa kumwaga tone la maji katika ardhi hii kavu. Leo kama Wasalvatoriani tuna utume mkubwa sana ulio mbele yetu. Tutasambazaje utume wetu wa Kisalvatoriani kwa kusoma alama za Nyakati? "

"Roho yetu ya ukumbakumba unaonyeshwa kwa namna na njia zote ambazo zitaangaziwa kwa upendo wa Mungu."

Sheria # 8

"Mashirika ya maisha ya walio wakfu yanaombwa kujiamini na kuanzisha upya ujasiri wa uanzishaji, ubunifu na utakatifu wa Waanzilishi wao kuendana na alama za nyakati zinazojitokeza katika ulimwengu wa leo. Mwaliko huu mwanzo wa yote ni mwito wa uvumilivu katika njia ya utakatifu katikati ya magumu ya kimwili na kiroho ya maisha ya kila siku. Lakini pia ni wito wa kufuatilia utaalamu katika shughuli binafsi na kukuza uaminifu endelevu katika utume, kuendana na mitindo, kama kuna hitaji, katika mazingira mapya na mahitaji tofauti, kwa uwazi mkubwa wa msukumo wa Mungu na kwa utambuzi wa Kanisa. "Lakini wote ni lazima waeleweshwe kwa kiasi kikubwa kwamba jitihada za kutafuta kuendana na Bwana ni dhamana ya kujifanya upya ambayo inahitaji kuwa waaminifu kwa msukumo wa asili wa shirika. Katika roho hii kuna hitaji la muhimu kwa siku hizi kwa kila shirika kurudi katika sheria, kwa kuwa sheria na katiba inatuonyesha ramani ya safari nzima ya ufuasi. Kutokana na karama ya pekee iliyothibitishwa na Kanisa. Heshima kubwa kwa sheria haitawaangusha watu walio wakfu kutoa vigezo vinavyotakiwa katika jitihada zao za kutafuta mtindo wa maisha unaofaa wa ushuhuda ambao utawawezesha kuendana na mahitaji ya nyakati bila kutoka nje ya msukumo wa awali wa shirika.[1]

"Tunajifunua kwa Maswali na Changamoto za Kipindi Chetu cha Kihistoria, kwa kuruhusu alama za nyakati zitufunulie njia na namna ya kuendana nazo."

Sheria # 8a

Baba Jordani alikuwa ni mtu mwenye uelewa mpana. Mtazamo wake wa kitume ulikuwa ni kwa ulimwengu mzima. *"Kama kuna mtu mmoja duniani ambaye hamjui Mungu na hampendi kuliko vitu vyote, msijipe hata kidogo muda wa mapumziko…"*[2]

---

[1] Vita Consecrata, 37

[2] Kumbukumbu ya Kiroho II, 1 - 2

Huu ni utume wetu ambao Wasalvatoriani wanatakiwa kuupeleka katika pembe zote nne za ulimwengu.

"Kuwa mtume wa kweli wa Yesu Kristo. Msipumzike mpaka mmepeleka neno la Mungu katika kona zote za dunia. Muwe wajumbe wa kweli wa aliye juu! Mpae kama tai ulimwenguni kote na kutangaza neno la Mungu."[3]

Ili kuwa wajumbe wa kweli katika kona nne za ulimwengu Baba Mtakatifu wetu Fransisi anawaomba Mapadre na Watawa kutafakari jinsi mwokozi alivyotoka nje, jinsi alivyohubiri, jinsi alivyoona ulimwengu. Ni lazima uwe utume halisi ambao unaongea kwa uhakika kwa kila Msalvatoriani. Sisi Wasalvatoriani ni lazima tujiandae kumfuata Yesu Mwokozi bila kujibakiza.

"Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu; mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima, wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango, nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni."[4]

Muono wa Alama za Nyakati kwa WanaSayansi Jamii

Katika karne ya 18 na hata kabla, kulikuwa na wataalamu wengi wa mambo ya jamii, ambao walileta maana mpya ya jamii. Wao pia walifahamu juu ya alama zao za nyakati. Jitihada yao ilikuwa ni kujenga jamii nzuri na kudumisha maadili mema ambayo yalikuwa yanafifia taratibu katika jamii zao kwa wakati ule. Mmoja wa wataalamu hao wa mambo ya kijamii, aliitwa Emil Durkheim, ambaye alionyesha kwamba jamii imekuwa ni jamii isiyo na sheria. Na hii ndio ilikuwa sababu kubwa kwa mauaji. Alianzisha neno maalumu "anomie," lenye maana ya enye kutokuwa na viwango vya kijamii au maadili.[5]

Utamaduni wa Kiasia

Sisi ni Waasia! Kimsingi Asia ni ulimwengu wa kidini wenye mila na desturi. Lakini kuna tabu na umaskini wa hali ya juu. Ni nani anawajibika na hili? Kutokana na sababu mbalimbali kuna matatizo mengi yanayoibuka kwa siku za leo. Lakini sasa limekuwa ni tatizo la ulimwengu mzima. Kwa hiyo ni muda wetu wa kujiandaa kutatua matatizo haya na kumweka Yesu Kristo katikati ya kila mmoja. Utume wetu unatupa changamoto na unatudai sana. Kutokana na Neno la Mungu na Baba Jordani ni lazima kujitayarisha na kuwa tayari kwa kila kitu. Halafu utume wetu wa Kisalvatoriani utakuwa hai ulimwenguni kote.

Tunajivunia kuzaliwa Asia, sehemu ambapo dini zote kubwa zilizaliwa hapa. Ingawa Waasia wengi ni maskini, mila na desturi zetu ni tajiri. Zinatusaidia kujenga uhusiano na Mungu, na watu wengine na pia ulimwengu mzima. Mila na desturi zetu zinaimarisha dini za watu wetu hata katika nyakati za kisasa. Zaidi ya hapo makanisa yetu yamejaa waamini wengi wa Kikristo. *"Katika mazingira ya Kiasia, matendo ya kiutamaduni na kidini ya Maskini inaweza ikawa chanzo tajiri kufanya upya karama. Pale tunapopaza sauti na maskini katika maisha yao ya kiroho na kutambua maadili na asili yao – unyoofu wa maisha, uwazi wa kweli na ukarimu wa pamoja, kipao mbele*

---

[3] Ibid no. 1/182.3

[4] Mt. 5: 13 - 16

[5] Wataalamu wa Elimu ya Sayansi ya Kijamii – Lewis A. Coser

kwa jumuiya, utii kwa familia na heshima kwa wazee – yanaweza yakapongezwa na kutangazwa kama maadili halisi ya Injili haijalishi kwa dhehebu gani la kidini maskini hawa wanatoka."[6]

Kutokana na tamaduni zetu za Kiasia familia zetu zipo karibu sana na tuna jamii yenye mfumo dume. Katika jamii hii kila mtu huheshimu wazee wao na wanawake pia wanalindwa. Lakini kupitia utandawazi kuna maendeleo ya haraka katika jamii ya leo kiuchumi, kisiasa, kijamii kutokana na utamadunisho. Zaidi ya hayo, watu hawawezi kustahimili mifumo yao migumu ya maisha kwa sababu ya umaskini na mabadiliko ya jamii. Kwa hiyo wengi wanahama wakitafuta malisho bora ya mifugo kwa ajili ya kukua kiuchumi. Je, wanapata kweli hayo malisho ya kufikirika? Badala yake kuna mateso makubwa na nyumbani kuna mateso makubwa yanayotokea katika maisha ya familia. Kutokana na umaskini wa watu wetu wanakuwa katika hali ya kusikitisha katika maisha yao kama vile ukahaba, uhamaji, vita, unyanyasaji wa watoto, utoaji wa mimba n.k. Kama Wasalvatoriani utume wetu halisi ni kuwa na utambuzi wa alama za nyakati.

"Mungu aliupenda ulimwengu hivyo kwamba alimtoa mwanae wa pekee kama mwokozi. Akisukumwa na mahitaji makubwa ya watu kutafuta uzima na kumjua Mungu wa kweli tu na Yesu Kristo ambaye alimtuma Fransis wa Msalaba na Maria wa Mitume kuanzisha shirika letu." [7]

Mshikamano kama Wito wa Msingi kwa Utume wa Wasalvatoriani

Utume wa Wasalvatoriani unamtaka kila mmoja wetu awajibike ipasavyo. Papa Yohani Paulo wa II aliongelea juu ya mgawanyo wa Kaskazini – Kusini. Pamoja na mgawanyo kati ya ulimwengu wa kwanza (nchi matajiri sana) na ulimwengu wa tatu (nchi maskini sana). Tunapotumia mgawanyo huu kwetu, kwa kujua na kwa kuona hali halisi katika jamii yetu, tukiwa na roho ya mwanzilishi wetu ni lazima tuwe na upendeleo kwa watu maskini. Ni lazima tuwe na mshikamano nao.

Kuwa katika mshikamano ni moja kati ya sifa zetu kuu kama Wasalvatoriani. Hasa sisi tunaoishi katika nchi za ulimwengu wa tatu ni lazima tuwe wamoja pamoja na wale wanaotuhitaji. Moja ya Barua ya kichungaji inayohusiana na mafundisho ya Kijamii ya Papa Yohani Paulo wa Pili, *Solicitudo Rei Socialis* (kuhusiana na mambo ya jamii ya kanisa) kwa kiasi kikubwa inaongelea kuhusu mshikamano. Baba Mtakatifu alipenda kuongelea juu ya mshikamano na ulimwengu mzima kupitia barua hii ya kichungaji. Imeongolea kwa mapana juu ya ufa kati ya matajiri na maskini.

"Mshikamano ni jibu linalofaa kwa hali ya kutegemeana na hitaji la kuondoa ufa uliopo kati ya matajiri na maskini."[8]

"ujumbe wa mafundisho ya kanisa juu ya mambo ya jamii, kuhusiana na mshikamano unaonyesha wazi kwamba kuna muungano wa karibu kati ya mshikamano na faida kwa wote, kati ya mshikamano na kikomo cha ulimwengu wa mema, kati ya mshikamano na usawa kati ya watu kwa ujumla, kati ya mshikamano na amani katika ulimwengu."[9]

---

[6] Mambo ya Msingi ya Kisalvatoriani Sehemu ya 2 ukurasa 113
[7] SDS W. RoL #2
[8] Solicitudo Rei Socialis 38 - 39
[9] Muhutasari wa Mafundisho ya Kanisa juu ya mambo ya kijamii, 194

Kupitia mshikamano tunaleta umoja kati ya watu wote. Mara zote ni njia inayotuelekeza kwenye amani. Mshikamano inawakumbusha wanashirika kutambuana kama watu na sio kama vyombo au njia. Kama Wasalvatoriani inatusaidia sana kuhudumia mahitaji ya wote, hasa wanaonyonywa na waliotengwa.

Kwa uhakika mshikamano ni fadhila ya Kikristo na kwa namna hiyohiyo ni fadhila kwa binadamu wote. Kwa upande mwingine ni majiltoleo ya mtu kwa faida ya wote.

"Wema kwa wote haupo katika ujumla wa kila mtu binafsi katika kizio cha jamii. Kuwa kwa wote na kwa kila mtu binafsi ipo na inabaki kuwa "pamoja" kwa sababu haugawanyiki na kwa sababu ni kwa pamoja tu tunaweza kupata, kuongeza na kulinda ufanisi wake, kuhusiana pia na wakati ujao."[10]

Faida ya pamoja ni lazima ifanywe kwa ukamilifu wake. Inasaidia kuwezesha uwezo na utu wa watu. Haki na wajibu wa mtu mmoja mmoja na makundi ni lazima yalinganishwe chini ya faida ya pamoja. Ni lazima tuwe na ujasiri wa Kisalvatoriani kupambana na alama hizi kama mwanzilishi wetu Baba Fransis Jordani. Yeye alikuwa ni mtu aliyemfuata Yesu kwa ukamilifu. Kama anavyosema:

"Mimi hapa, nitume kwa ajili yako, kwa ajili ya roho, kwa ajili ya Kanisa la Mungu. Yote, ee baba, yote, yote ee Mungu, yote, Ee Yesu, yote, ee mwokozi wa ulimwengu, ninatamani kwa moyo wote kuwaokoa wote! Oo, okoa roho! Oo okoa roho! Ninakuomba na kukusihi sana, okoa roho! Igharimu kiasi chochote kile, okoa roho!"[11]

Maadili ya Kikristo kwa Wasalvatoriani

Maadili ya Kikristo yanatolewa kwa ufupisho mzuri sana na barua kwa Wakolosai: *"Basi ikiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu. Basi vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi: uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu."*[12]

"Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri"[13]

Hitimisho

Katika ulimwengu huu wa sasa ni lazima tupeleke tunu hizi za maadili kwa watu. Maadili haya ni lazima yawe ni majibu kwa alama za nyakati za leo. Baba Jordani alijaribu kwa jitihada zake zote kuleta maadili mema katika jamii. Alipigana mara kwa mara kuleta uhalisia kwa jamii, ambazo zilikuwa zinakwenda mrama kwa kipindi hicho. Leo pia tunaweza tukaona dalili nyingi za umaskini, utofauti wa usawa, na ukosefu wa maadili kwa maisha ya watu. Watu wengi wanatafuta utu wao ambao hawana. Katika jamii baadhi ya watu wanapigana kwa ajili ya haki na wajibu wao. Huo ndio uhalisia wa ulimwengu wa leo na huu ndio muda wetu mwafaka wa kupaza sauti zetu

---

[10] Ibid Sura ya 4, 164
[11] Kumbukumbu ya Kiroho (SD) II/12.
[12] Kol. 3:1-6
[13] Mt. 19:17

za kinabii kama Wasalvatoriani; na kwa njia hiyohiyo ni lazima kuleta maisha ya kiroho ya Wasalvatoriani katika jamii na kwa wahitaji.

Manabii wa Biblia walisukumwa na haki na kila wakati walipaza sauti zao dhidi ya udhalimu. Walileta mshikamano na wote: *"Ufahamu wa Manabii uliwaimarisha wanyonge katika kutafuta faida ya pamoja na uimarishaji mpya wa haki."* [14]

Yesu pia alipaza sauti yake dhidi ya udhalimu na kutengeneza jamii mpya. Alitambua pia alama za nyakati. Yesu alifanya kazi kubwa kwa mabadiliko ya muundo katika jamii yake. Sala na kufunga ilikuwa ndio njia yake. Baba Jordani alikuwa pia na utume wa kinabii katika maisha yake. Alimfuata Yesu Mwokozi na alikuwa mtu wa sala. Tukimuiga yeye ni lazima tujiweke katika uhusiano mkuu na Yesu, Mwokozi.

"Unapofanya jambo lolote la muhimu wakati wowote ule ambalo ni zuri na lenye manufaa, lijaribu ikiwa pia unaweza ukajitenga kwa masaa machache kwa tafakari pamoja na Mungu, kabla ya kujitoa kwa moyo wote kwa ajili hiyo."[15]

Halafu Mungu anatupa nguvu na ujasiri kuwa na mshikamano na wahitaji, na kupaza sauti zetu dhidi ya udhalimu. Sisi kama Wasalvatoriani kutoka Asia, wajibu wetu mkubwa ni kuwainua maskini, kuwa na mshikamano nao. Hatutaweza kamwe kuwa na miundo na desturi ambayo haitufai kwa siku hizi. Kama Wasalvatoriani ni lazima tuchukue hatua madhubuti inayotupeleka mbele kwenye njia kamili kwa utume wetu, kusoma alama za nyakati.

"Yote kwa utukufu mkuu wa Mungu na kwa ajili ya wokovu wa roho."[16]

Maswali ya Tafakari

1. Soma tena Sheria za Familia ya Kisalvatoriani kwa mwanga wa makala hii.
    a. Onyesha maneno au misemo ambayo inakugusa na ujiulize, "jambo hili linaniambia nini mimi na nitalipa mwitikio gani?"
    b. Manufaa yake yanaweza kuwa ni yapi katika familia ya Kisalvatoriani katika eneo lako la ulimwengu au/na kwa ulimwengu mzima?
2. Kwa mwanga wa makala hii, kama ukiamua kuitengeneza upya sheria ya familia ya Wasalvatoriani, Je, Utaongeza kitu gani au kukibadili?
3. Mwandishi ameandika juu ya kuendana na alama za nyakati kutoka katika mtazamo wa Waasia na Wataalamu wa Sayansi ya Jamii. Je, unaweza ukawa Msalvatoriani wa kutoka Asia au hapana? Baada ya kusoma makala hii elezea juu ya maadili ya tamaduni za Waasia ambazo zinaweza kusaidia kuboresha utume wetu wa Kisalvatoriani kwa pande zote za ulimwengu.

---

[14] Baba Jordani: Nabii Kutoka Ujana Wake – Baba Milton Zonta, SDS
[15] SD I/65
[16] SD I/67